


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE



TAARIFA KWA UMMA

MTIHANI WA KUHITIMU ELIMU YA MSINGI MWAKA 2023.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe Ndugu Kuruthum Sadick ,anapenda kuwataarifu wananchi wote kuwa Jumla ya shule za msingi 95 zilizopo Halmashauri ya Mji Njombe zimekamilisha maandalizi kwa ajili ya mitihani ya darasa la saba ya kuhitimu Elimu ya Msingi mwaka 2023.

Idadi watahiniwa kwenye Shule za Msingi zilizopo Halmashauri ya Mji Njombe ni 4,871,kati yao wavulana ni 2,349 na wsichana ni 2,522.

Mitihani ya darasa la saba ya kuhitimu Elimu ya Msingi itafanyika kuanzia Tarehe 13 Septemba na kumalizika Tarehe 14 Septemba 2023.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe pamoja na Baraza la waheshimiwa madiwani tunapenda kuwatakia mtihani mwema watahiniwa wote wa darasa la saba kwa mwaka 2023.

Kila la Kheri ,Mkafanye Vuzuri kwenye mitihani yenu.

Kuruthum A. Sadick

Mkurugenzi.

Halmashauri ya Mji Njombe.

12 Septemba 2023

Ofisi ya Mkurugenzi (TD), S.L.P 577 NJOMBE, Tovuti: www.njombe.go.tz, Simu: 026-2968833

Barua pepe: td@njombec.go.tz, Posti Kodi : 31 Barabara ya Ikisa, 59108 Mjimwema -Njombe